



"If men just stopped raping us, rape will stop."

– Adelle Onyango (Kenyan radio presenter, social activist and media personality)

Pat's Story

Pat is a 12-year-old student from a Justice Club school in Nairobi. Pat was defiled repeatedly by a male teacher while attending class on a Saturday when only a few students were in school. Pat attended Justice Club activities and was empowered to report the incidences of defilement, informed his parents and was quickly taken to hospital and subsequently to Kilimani Police Station, a 160 Girls trained station. The teacher was arrested by the police and he is now in custody awaiting prosecution. It is alleged the teacher had defiled several other students. This matter is being investigated. *Note: Pat is not his real name.*



Shaming Survivors of Sexual Violence

When someone commits a rape, they will sometimes try to get away with it by blaming their victims. Community members may also blame rape survivors for being raped. However, **a rape survivor is never to blame (legally or morally) when a perpetrator rapes them.** It does not matter what the survivor was wearing, if they were drunk or on drugs, if they were friends with the perpetrator or didn't defend themselves "enough." People might blame survivors for acting "recklessly" if they choose to walk outside at night. However, no matter what, the perpetrator is responsible for the rape, not the survivor.

Impunity for Rape

Perpetrators of defilement can get away with their crimes more easily if community members, the police and the legal system believe that the child provoked the adult to violate them. However, children cannot legally consent to any sexual acts, and rape survivors cannot be held responsible for their rape. When a survivor is blamed, the perpetrator is not held accountable. **They can continue to perpetrate these horrible crimes because, in a culture of impunity for rape, they know that they will not be held responsible for their actions.** The social stigma surrounding sexual violence can sometimes make a survivor believe that they "wanted" to be assaulted, or that they asked for it accidentally. In many societies that condone rape culture, there is an idea that women provoke men to rape and that men are entitled to sex if they are married to the woman or girl, or if they have given their survivor a gift.



People say to only go out with people you trust to avoid being assaulted. However, because so many perpetrators are known relatives or friends of their survivors, this idea can make it almost impossible to protect yourself. It is not the responsibility of the survivor to avoid being raped. **It is the responsibility of the perpetrators not to rape or assault people in the first place.**



Perpetrators are to Blame

Sometimes, people will be raped multiple times by the same perpetrator. They will blame themselves for this because they feel as though they should know better after it has happened once. However, perpetrators will manipulate their survivors to make them believe that they must continue to assault them. People might feel like they have no choice but to comply with the abuser. They are scared and don't want to put their family in danger. They feel ashamed and don't want anyone else to know about it because they're worried that people won't believe them, or they will blame them for not better protecting themselves. It is very scary to be put in this position. **Survivors must not blame themselves and should feel confident to report the perpetrator and his crimes.**

COMMUNITY CORNER

This week we asked the Justice Club leaders: *What would you say to a survivor of defilement who feels scared, ashamed or guilty after a perpetrator has defiled them?*



Diligent Impala from Kakamega:

"I will make them understand that it was never their fault and that they should speak up to get justice."

Helpful Champion from Mombasa:

"I know you feel scared and ashamed but that is not the end of the world to you. You still have life and a bright future coming."



Loyal Panda from Nairobi:

"I would advise them to be confident that they will acquire justice and that it wasn't their fault that they were assaulted."

Fantastic Aardvark from Mombasa:

"[The survivor] should not worry or feel ashamed instead the perpetrator is the one to feel so because she/he is the wrong one in that matter and [the survivor should] continue with his/her life with full of confidence, dignity and respect."



To Report a Defilement

To download the free **160 Girls defilement reporting app**: scan the QR code (right) by pointing your phone's camera at the code. The app's web page will appear with an option to download the app. You can also search "160 Girls app" in your phone's app store or submit a "help request" on 160girls.org.



You can also connect with your local rape rescue partners:

KARE (Kakamega)

Tel: 0724721671/0721782381
E-mail: kare.org@gmail.com
Website: karemp.org

GVRC (Nairobi)

Tel: 0713513141/0719638006
E-mail: gvrc@nwch.co.ke
Website: gvrc.or.ke

ICRH (Mombasa)

Tel: 0722208652/0734466466
E-mail: info@icrhk.org
Website: icrhk.org

They can offer support, and help you report the defilement to the police. You can also report to the police on your own, or talk to a trusted friend or relative.






"Ikiwa tu wanaume wangekoma kutubaka, basi ubakaji ungekwisha."

- Adelle Onyango (Mtangazaji wa redioni, mwanaharakati wa kijamii, na pia mwanahabari)



Kisa cha Pat

Pat ni mwanafunzi wa miaka 12 kutoka mojawapo ya shule za Justice Club Jijini Nairobi. Pat alinajisiwa na mwalimu wake wa kiume kwa mara kadhaa alipokuwa akihudhuria masomo ya Jumamosi wakati ambapo wanafunzi wachache sana huwa shuleni. Pat alipohudhuria shughuli za Justice Club, alipata motisha na nguvu za kuripoti kisa cha kunajisiwa kwake. Kisha aliwafahamisha wazazi wake na mara moja akapelekwa hospitalini na baadaye katika kituo cha polisi cha Kilimani, ambacho ni mojawapo ya vituo vilivyopewa mafunzo na mradi wa 160 Girls. Mwalimu husika alikamatwa na polisi na kwa sasa yupo korokoroni akisubiri hukumu. Inasemekana kuwa mwalimu huyo amewanajisi wanafunzi wengine kadhaa. Kisa hiki bado kinachunguzwa. *Kumbuka: Pat sio jina la mhusika halisi.*



Kuwatia aibu Waathiriwa wa Dhulma za Kijinsia

Wakati mwingine mtu anapotenda unajisi atajaribu kujiondoa hatiani kwa kumlaumu yule aliyenajisi. Aidha, viongozi wa kijamii wanaweza kuwalaumu wale walionajisiwa. Hata hivyo, mwathiriwa wa unajisi hafai kulaumiwa (kisheria au kimaadili) pale anaponajisiwa. Haijalishi alivyovaa mwathiriwa, ikiwa alikuwa mlevi au katumia dawa za kulevya, ikiwa alikuwa na urafiki na yule aliyemnajisi, au hata hakujiipigania vya 'kutosha' ili kujiokoa. Huenda watu wakawalaumu waathiriwa eti kwa kutembea 'kiholela' gizani. Hata hivyo, aliye na kosa hapa ni yule anayetenda unajisi na wala si yule aliyenajisiwa.



Ukwepaji sheria kwa Wabakaji

Wabakaji wanaweza kukwepa adhabu ya kisheria kwa urahisi ikiwa wanajamii, polisi pamoja na mifumo ya kisheria itaamini kuwa watoto ndio walisababisha watu wazima kuwadhulumu. Hata hivyo, watoto hawawezi kupeana idhini yoyote kuhusu vitendo vya ngono, na kwamba waathiriwa hao hawawezi kuwajibikia dhulma walizotendewa na wabakaji. Ikiwa mwathiriwa atalaumiwa basi mbakaji husika hatawajibika. **Hivyo basi, mbakaji huyo anaweza kuendelea kutenda vitendo hivyo viovu kwani anajua atatenda ubakaji na kukwepa uwajibikaji wa vitendo vyake.** Unyanyapaa wa kijamii unaohusishwa na dhulma za kimapenzi unaweza wakati mwingine kuwafanya waathiriwa kuhisi kana kwamba ndio waliosababisha kitendo hicho au hata walitaka kutendewa hivyo bila kujua.



Katika jamii nyingi zenye utamaduni unaoruhusu ubakaji, kuna imani kuwa wanawake ndio wanaosababisha wanaume kuwabaka na kwamba wanaume wana haki kupata ngono ikiwa wameoa mwanamke husika au ikiwa wamempa mwanamke au msichana huyo zawadi. Watu husema kuwa unafaa tu kujumuika na watu unaowaamini ili kuepuka kudhulumiwa. Hata hivyo, kwa kuwa wabakaji wengi ni jamaa au marafiki, dhana kama hii inaweza kufanya kujikinga kuwa hata vigumu zaidi. Si jukumu lake mwathiriwa kujiepusha au kujilinda kutokana na ubakaji. **Ni jukumu lake mbakaji kutobaka au kuwadhulumu au kuwashambulia watu.**

Wabakaji Wanafaa Kulaumiwa

Wakati mwingine watu hubakwa mara kadhaa na mtu yule yule. Huenda waathiriwa kama hawa wakajilaumu kwani watahisi kana kwamba walifaa kufahamu kutendeka kwa uovu huo pale kulipotokea kwa mara ya kwanza. Hata hivyo, wabakaji watawahadaa waathiriwa wao ili kuwafanya waamini kuwa ni lazima waendeleo kuwadhulumu. Huenda waathiriwa hao watahisi kwamba hawana jingine ila kukubali kile wanachokitaka wadhulumu wao. Wanahofia kuiweka familia yao katika hatari. Wanaona aibu na hivyo wasingetaka watu kufahamu kitendo hicho kwani wanadhani watu hao hawatawaamini au watawalaumu kwa kutojikinga inavyofaa. Inahofisha sana kujipata katika hali kama hii. **Waathiriwa hawafai kujilaumu na kwamba wanafaa kuwa wakakamavu na kumripoti mbakaji husika.**

Pembe ya Kijamii

Juma hili tuliwauliza viongozi wa Justice Club: Je, utamwambia nini mwathiriwa wa unajisi ambaye ana hofu, aibu na anayehisi kuwa anafaa kulaumiwa baada ya kunajisiwa?



Alisema Diligent Impala kutoka Kakamega:

“Nitamfanya kuelewa kuwa halikuwa kosa lake na kwamba anafaa kuzungumza kuhusu kisa hicho ili kupata haki.”

Alisema Helpful Champion kutoka Mombasa:

“Ninajua kuwa una hofu na pia aibu, lakini huu sio mwisho wa dunia kwako. Bado ungali na maisha mazuri ya siku za usoni.”



Alisema Loyal Panda kutoka Nairobi:

“Ningewashauri kuwa na imani kwamba watapata haki, na kwamba halikuwa kosa lao kudhulumuwa.”

Alisema Helpful Champion kutoka Mombasa:

“[Mwathiriwa] hafai kuhofia au kuona aibu. Badala yake, mbakaji ndiye anayefaa kuhisi hivyo kwani ndiye aliyetenda kosa, na kwamba (mwathiriwa anafaa) kuendelea na maisha yake kwa ukakamavu na heshima.”



Ili Kuripoti Unajisi:

Pakua (Download) app ya 160 Girls inayohusu kuripoti visa vya unajisi (160 Girls defilement reporting app): skana (scan) msimbo wa QR (QR code) - ulio upande wa kulia kwa kuumulika kwa kamera ya simu yako. Wavuti (website) ya app hiyo itafunguka na kuashiria ‘Download’. Vilevile unaweza kuitafuta app hiyo kwenye app store yako au kutuma ombi kwa 160girls.org



Unaweza pia kushirikiana na wadau wa unajisi waliokaribu nawe:

KARE (Kakamega)

Tel: 0724721671/0721782381
E-mail: kare.org@gmail.com
Website: karemp.org

GVRC (Nairobi)

Tel: 0713513141/0719638006
E-mail: gvrc@nwch.co.ke
Website: gvrc.or.ke

ICRH (Mombasa)

Tel: 0722208652/0734466466
E-mail: info@icrhk.org
Website: icrhk.org

Hawa wanaweza kukupa msaada pamoja na kukusaidia kuripoti unajisi huo kwa polisi. Vilevile, unaweza kuripoti kwa polisi mwenyewe au kumweleza rafiki au jamaa yako.

